**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

**2025**

**Dodoma**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA KILOSA**

SHULE YA SEKONDARI KIMAMBA,

S.L.P. 66**,**

**KIMAMBA.**

**22/04/2025**

KUMB.Na. **KSS/JI/1/FV/2025/2026**

**NAMBA ZA SIMU:**

MKUU WA SHULE: 0782866776/0620555751

MAKAMU MKUU WA SHULE: 0755315022/0622146365

MATRON/PATRON: 0712040885/0752800630/0766978804/0717297237

**MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI ………….**
**……………………………………………..........**
**S.L.P ……………………………………..........**
**……………………………………………..........**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KIMAMBA HALMASHAURI YA WILAYA YA KILOSA MKOA WA MOROGORO MWAKA 2025**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2025 na atasoma tahasusi ya ………….

Shule ya Sekondari Kimamba ipo Wilaya ya Kilosa Mkoa wa Morogoro.Unapokuja shule ya sekondari Kimamba ufike Morogoro mjini utapanda magari ya Kilosa kupitia njia ya Mkata au Dumila (kwa atakaepitia

njia ya Dumila apande magari yanayopita Kimamba) utashuka stendi ya Kimamba. Shule ipo jirani kama mita 200 kutoka stendi.
Utakayesafiri kwa gari – moshi (Train) unashauriwa ushuke stesheni ya Kimamba.
Muhula wa Masomo unaanza tarehe 08/07/2025 hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 07/07/2025 Mwisho wa kuripoti ni tarehe 08/08/2025

## 2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA:-

### 2.1 SARE ZA SHULE

a) Sare ya shule hii ni suruali ya kitambaa chenye rangi ya damu ya mzee (**maroon)** isiyo na mishono ya kihuni, yenye turn up upana chini sm16, shati jeupe lenye mikono mifupi (WAVULANA) hivyo aje na suruali mbili na mashati mawili.

b) Sketi ya kitambaa rangi ya damu ya mzee (**maroon)** yenye rinda moja lenye mshono wa V kwa mbele (**SKETI HIYO IWE NDEFU KARIBU YA KUGUSA KISIGINO, SKETI FUPI HAZITAKIWI).** Shati jeupe lenye mikono mifupi (WASICHANA), aje na sketi mbili na mashati mawili.

c) Rangi ya Hijab (kijuba) ni lazima ifanane na sare ya shule (yaani kitambaa cheupe)ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama.

d) Sare ya Michezo kwa shule hii ni jezi ya Timu ya Taifa(rangi ya Bluu) au track suit ya bluu kwa wasiovaa bukta kwa wavulana na wasichana, pia aje na raba kwa ajili ya michezo.

e) Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;

f) Soksi jozi mbili nyeupe zisizokuwa na maandishi.

g) Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali;

h) Sweta rangi ya damu ya mzee lifanane na rangi ya suruali/sketi kwa ajili ya kujikinga na baridi wakati wa kipupwe.

i) Sare za kushindia ni: suruali ya dark blue (wavulana), sketi ya dark blue ya malinda ndefu karibu ya kugusa kisigino (wasichana) na T – shirt ya njano (**T – shirt zinapatikana shuleni**).

j) **Tai itapatikana shuleni**

### 2.2 MAHITAJI MENGINE MUHIMU AMBAYO MWANAFUNZI ANAPASWA KUJA NAYO SHULENI:-

i. Madaftari 6 (counter books Q3) ya notes, mathemitical set, rula na kalamu za kutosha.
ii. **Ream (A4) mbili** (2) kwa mwaka;
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (*orodha imeambatanishwa*);
iv. Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma Biology;
v. Scientific Calculator;
vi. Godoro la upana wa futi mbili na nusu kwa ajili ya kulalia.
vii. Mashuka Jozi 2 rangi ya light blue au pink yasiyokuwa na maua au maandishi, foronya ya godoro 1, chandarua 1 (*nyeupe);*
viii. Nguo za ndani za kutosha;
ix. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
x. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;
xi. Kwanja 1 wote, jembe 1 na mpini wake wote,( reki 1 kwa PCM), (rubber squeezer1 kwa PCB), (soft bloom1 kwa CBG), Brush ya choo 1 wote na chelewa yenye mshikio 1 wote) .
xii. Sanduku kubwa la bati Trunker) kwa usalama wa vifaa vyake.
**xiii. Photocopy ya result slip.**
**xiv. Photocopy ya cheti cha kuzaliwa**

**2.3 MICHANGO MBALIMBALI**

**SHULE ZA BWENI**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

Fedha hizo zilipwe kwenye akaunti ya shule. Jina la akaunti ya shule ni **KIMAMBA SECONDARY SCHOOL REVENUE COLLECTION ACCOUNT.** Akaunti nambari **21801000011** katika benki ya **NMB.** (**Tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye paying slip nakala aje nayo shuleni wakati wa kuripoti)**

**NB. FEDHA MKONONI HAZITAPOKELEWA.**

**3. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia

mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

## 3.1 SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**
- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**
- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

## 3.2 MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE NI PAMOJA NA:

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;

iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara/bangi;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.


**4. VIAMBATISHO NA FOMU MUHIMU**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**5.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Saini ya Mkuu wa Shule**



**Jina la Mkuu wa Shule: MANSETUSY K. NGASWA**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule**

HEADMASTER
KIMAMBA SECONDARY SCHOOL
KILOSA

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule: 0782866776/0620555751**
- **Makamu Mkuu wa Shule:** 0622146365/0755315022
- **Mwandamizi Taaluma: 0655281120/0655635758**
- **Mwandamizi Malezi: 0787783702/0676344783**

## 6. VIAMBATISHO NA FOMU MUHIMU

### a) Medical examination form

**THE PRESIDENT'S OFFICE**
**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**
**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

**FROM: THE HEADMASTER**
**KIMAMBA SECONDARY SCHOOL**
**P.O.BOX 66**
**KIMAMBA**

HEADMASTER
KIMAMBA SECONDARY SCHOOL
KILOSA

**TO: THE MAEDICAL OFFICER**

……………………………….
……………………………….
……………………………….
……………………………… (Name in full) please examine the above named Student as to hi/her physical and mental fitness for a full time student. The examination should include the following:-

a. (i) Eyesight…………………………………
(ii) Hearing…………………………………
(iii) Speech…………………………………..
(iv) Limbs……………………………………
(v) Veneral diseases……………………...
(vi) Leprosy…………………………………
(vii) Epilepsy…………………………………
(viii) Spleen…………………………………...
(ix) Abdomen………………………………...
(x) Urine……………………………………...
(xi) Stool……………………………………..

b. Neurosis…………………………………

c. Other serious disease e.g.
i. Asthma ……………………………..
ii. TB ………………………………….

d. Pregnancy……………………………………..

(To be completed by a government medical officer) I have examined that above named student and consider that he/she is fit/unfit for a full time studies.

Name……………………………………
Date ………………………………..
Signature ………………………

### 7. Fomu ya maelezo binafsi

| |
|---|
| **PICHA** |

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**SHULE YA SEKONDARI KIMAMBA**

**FOMU YA TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI KUKUBALI SHERIA NA NAFASI YA SHULE ALIYOPANGIWA**

**A. TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI:-**

- JINA LA MWANAFUNZI ………………………………………….
- MAHALI ALIPOZALIWA (MKOA/MTAA)…………………………….
- ANAISHI/MNAKAA WAPI (KATA/MTAA)
- URAIA: MTANZANIA/SIYO MTANZANIA………………………
- SHULE ALIYETOKA……………………………………………….
- NAMBA YA MTIHANI (CSEE)……………………………………….....

**B. TAARIFA YA MZAZI /MLEZI:-**

- JINA LA MZAZI/ MLEZI…………………………………………….
- KAZI YA MZAZI/MLEZI…………………………………………….
- ANUANI YA MZAZI/MLEZI…………………………………………
- SIMU YA MZAZI MLEZI……………………………………………
  - KAZINI……………………………
  - NYUMBANI………………………
  - MKONONI……………………..
  - AU KAMA HUNA: NAMBARI YA SIMU YA JIRANI YAKO NI…………………

**C. KUKUBALI NAFASI NA MAELEKEZO ULIYOPEWA:**

Mimi………………………………………kidato……………..Mwaka……………...

Nimesoma ka kuyaelewa maelekezo yote. Kwa hiyo nakubali kuipokea/sikubali kuipokea nafasi niloyopewa. Nathibitisha kwamba nimepokea maagizo na maelekezo bila kulazimishwa naahidi kuyazingatia.

Tarehe……………………………… Saini……………………………….

**D. KUKUBALI SHERIA ZA SHULE**

**MWANAFUNZI:**

Mimi…………………………………………………………………………nimezisoma na kuzielewa sheria za shule na naahidi kwamba nitazingatia na kutii masharti, sheria za shule na maelekezo mengine nitakayopewa na waalimu na viongozi wote wa shule. Nikikiuka sheria hizo, hatua za kinidhamu zichukuliwe dhidi yangu kwa mujibu wa kanuni, taratibu na sheria zilizopo.

Tarehe………………………………………Saini………………………………..

**E. MZAZI/MLEZI (AJAZE SEHEMU HII)**

i. Mimi mzazi/mlezi wake nathibitisha kuwa mwanangu ……………………………….
Ameelewa maagizo na ninapenda ifahamike kuwa dini ya mwanafunzi ni ……………………..madhehebu yake ni…………………………………….

ii. Ninaruhusu/ siruhusu mwanangu kushiriki katika makongamano au warsha Za kidini nje ya shule pasipo kuwa na mwalimu mlezi wa shule hii.

iii. Aidha mimi ………………………………………………………… ambaye ni Mzazi/mlezi nimesoma sheria na maagizo mengine ya shule yanayomhusu mwanafunzi………………………………………………. na ninaahidi kutimiza wajibu wangu nikiwa mzazi/mlezi wa mototo huyu kwa kumshauri ipasavyo Pamoja na kumtimizia mahitaji yake ya shule.

**JINA LA MZAZI/MLEZI…………………………………………………………**

**NAMBA ZA SIMU…………………………………………………….**

**SAHIHI YA MZAZI/MLEZI…………………………………………..**

**TAREHE …………………………………..**

C) Picha mbili (PASSPORT SIZE) za mwanafunzi na picha nne(PASSPORT SIZE) za wazazi 2 na ndugu 2 wa karibu wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni Pamoja na namba zao za simu.

## ORODHA YA VITABU


### GEOGRAPHY

1. PRITCHARD JM (1976). FIRST LESSON IN MAP READING EAST AFRICA, London
2. Goh Cheng and Gillian C. Morgan (1982). HUMAN AND ECONOMIC GEOGRAPHY (2nd edition). Great Clarendon Street, Oxford OX2 6DP.
3. R.B Bunneth (1973) GENARAL GEOGRAPHY IN DIAGRAMS (1st edition). Person Education South Asia Pte Ltd.
4. Zist kamili (2010). PRACTICAL GEOGRAPPHY ALIVE (2010 version). KOT PUBLISHERS
5. Zist kamili (2010). PHYSICAL GEOGRAPPHY ALIVE (2010 version). KOT PUBLISHERS
6. Zist kamili (2010). REGIONAL GEOGRAPPHY ALIVE (2010 version). KOT PUBLISHERS
7. DT Msabila (2003). A COMPREHESIVE APPROACH TO PHYSICAL GEOGRAPHY for secondary schools. Nyambari Nyangwine Publishers.
8. DT Msabila (2003). A COMPREHESIVE APPROACH TO PRACTICAL GEOGRAPHY for secondary schools. Nyambari Nyangwine Publishers.
9. DT Msabila (2003). A COMPREHESIVE APPROACH TO REGIONAL GEOGRAPHY for secondary schools. Nyambari Nyangwine Publishers.

### PHYSICS

1. V.K Mehta and Rohit Mehta (1998). PRINCIPLES OF PHYSICS, for class XI (1st Edition). S.Chand school books.
2. V.K Mehta and Rohit Mehta (1998). PRINCIPLES OF PHYSICS, for class XII (1st Edition). S.Chand school books.
3. Roger Muncaster 919973). A – LEVEL PHYSICS (4th edition). Oxford university press.
4. Tom Duncan (1973). ADVANCED PHYSICS (5th edition). Hodder Education, an Hachette UK Company.
5. Jim Breithaupt (2000). NEW UNDERSTANDING PHYSICS for Advanced Level (4th edition). Stanley Thornes (Publishers) Ltd.
6. Michale Nelkon and Philip Parker (1997). ADVANCED LEVEL PHYSICS. (7th editon). Books by Michael Nelkon published by Heinemann.
7. Understanding Mechanics,second edition. By A.J. Sadler & D.W.S Thorning.
8. Calculations for A – level physics T.L.Lowe and J.F.Rounce 4th Edition.

### GENERAL STUDIES

1. Richard R.F Mbalase (2011). GENERAL STUDIES FOR ADVANCED LEVEL (Certificate, form six).
2. Joannes Bigirwamungu and sospeter M Deogratias (2012). Understanding ADVANCED LEVEL GENERAL STUDIES (1st edtion). Mikumi publishers.
3. Nyambari C.M Nyangwine, Godfrey R Bukagile and Stephen O. Maluka. ADVANCED LEVEL GENERAL STUDIES NOTES form 5 & 6.

### BIOLOGY

1. Michael Kent (2000). ADVANCED BIOLOGY (1st edition). Oxford university press.

2. Sarita Aggarwal (2008). A TEXT BOOK OF CBSE BIOLOGY (1st edition). S. Chand and Company Ltd.
3. D.J. Taylor, N.O.P Green and G.W.Stout (1997). BIOLOGICAL SCIENCE (3rd edition) Cambridge university Press.

**CHEMISTRY**

1. En Ramsden (2014). A – LEAVEL CHEMISTRY (4th Edition). Oxford University Press.
2. Dr.S.K.Jain (2008).CONCEPTUAL CHEMISTRY (1st Edition). S.Chand and Company Pvt Ltd
3. Ted Lister and janet Renshaw (1991). NEW UNDERSTANDING CHEMISTRY FOR ADVANCED LEVEL (3rd Edition). Oxford University Press.

**BASIC APPLIED MATHEMATICS**

1. Tanzania Institute of Education (2009). "Basic Applied mathematics Syllabus for Advanced Secondary Education, Form V and VI". Ministry of Education and Vocational Training, Dar-es – Salaam.
2. BASIC APPLIED MATHAMATICS for Advanced secondary schools form V & VI By S.I. Sillem.

**ADVANCED MATHEMATICS**

1. Backhouse, J.K. Houldsworth, S.P.T., copper B.E.D (1985) PURE MATHEMATICS – 2 (4th edition). 90 Tottenham Court Road, London W1P9HE.
2. Backhouse, J.K. Houldsworth, S.P.T., copper B.E.D (1985) PURE MATHEMATICS – 1 (4th edition). 90 Tottenham Court Road, London W1P9HE.
3. Foard Pat (1998). ELEMENTARY STATISTICS A STEP BY STEP APPROACH.Mc Hill Companies, Inc.
4. Solomon R.C (2004). PURE MATHEMATICS (7th edition), John Murray (publisher) Ltd, London, NW1 3BH.
5. C.J Tranter (1975). ADVANCED LEVEL PURE MATHEMATICS (4th edition).Hoder & Stoughton, London.
6. H.K Dass and Dr. Rama Verma (2005). MATHEMATICS, for class XII, Volume – I,with value Based Questions (1st edition). S.Chand & Company PVT.LTD.
7. HK Dass (1988). ADVANCED ENGINEERING MATHEMATICS (1st edition) S.Chand & Company Pvt Ltd, Ram Nagar, New Delhi.
8. Understanding pure mathematics for advanced level.
9. HK Dass and Dr. Rama Verma (2005). MATHEMATICS for class XII, Volume- II, with value Based questions (1st edition). S. Chand & Company Pvt,Ltd.

RANGI YA SARE (SURUALI/SKETI)

